# MAPITIO YA MWENENDO WA SOKO KWA WIKI
# 7 FEBRUARI 2025

**KARIBUNI TENA KATIKA KIPINDI CHETU CHA KILA WIKI KINACHOKUHABARISHA KUHUSU MWENENDO WA SOKO LA HISA LA DAR-ES-SALAAM, NA KULETWA KWENU NA VERTEX INTERNATIONAL SECURITIES, PAMOJA NANYI LEO NI MIMI, FRANCO ATILYO**

Kwa wiki inayoishia tarehe 7 Februari 2025, mauzo katika Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) yaliohgezeka kwa asilimia 0.27 kutoka TZS 6.9 bilioni hadi TZS 6.94 bilioni. Lakini, kiasi cha hisa zilizouzwa kilipungua kutoka hisa milioni 6.95 hadi hisa milioni 5.3 sawa na asilimia 23.12.

Jumla ya Mtaji wa Soko uliongezeka kwa asilimia 2.39 kutoka TZS 18.53 trilioni hadi trilioni 18.97. Mtaji wa Soko la Ndani nao uliongezeka kwa asilimia 0.24, hadi TZS 12.60 trilioni kutoka TZS 12.57 trilioni kutokana na kuongezeka kwa bei ya hisa za ,CRDB, MKCB, na TCCL.

CRDB imeongoza kwa mauzo ya hisa wiki hii ikirekodi TZS 3 bilioni, ambayo ni 43.96% ya mauzo yote ikifuatiwa na NMB kwa asilimia 21.14 ya mauzo yote.

Kuhusu bei, hisa za CRDB ziliongezeka kwa TZS 20 wakati za DCB zilipungua kwa TZS 5 huku za MKCB zikiongezeka kwa TZS 20 na za TCCL zikiongezeka kwa TZS 100. Kwa upande wa hisa za NMB zilipungua kwa TZS 50 huku za NICO zikipungua kwa TZS 40

CRDB iliongoza kwa idadi ya kubwa ya hisa zilizouzwa kwa asilimia 81.52 sawa na hisa milioni 4.4 ikifuatiwa na TCC kwa asilimia 6.19. Jumla ya hisa milioni 1.72 za CRDB, TCC na NMB ziliuzwa kupitia kaunta ya makubaliano ya kabla huku wawekezaji wa nje wapungua kiasi wiki hii. Tunatarajia kuongezeka kwa mwitikio utakaoakisi kwenye mauzo ya hisa na bei kwa wiki zijazo.

Katika wiki kulikuwa na miamala 76 kwenye soko la hatifungani, ambapo soko lilisajili takribani TZS 37.49 bilioni.

Mnada wa hatifungani ya Serikali ya miaka miwili namba 668 uliofanywa na Benki Kuu ya Tanzania tarehe 5 Februari 2025, ulisajili zabuni 72 ambapo zabuni 17 zilifanikiwa na kukusanya kiasi cha TZS 24.6 bilioni.

# MAPITIO YA MWENENDO WA SOKO KWA WIKI
# 7 FEBRUARI 2025

**MPAKA HAPO TUMEFIKIA MWISHO WA MAPITIO YA SOKO LA HISA LA DAR ES SALAAM KWA WIKI ILIYOISHIA IJUMAA YA FEBRUARI 7, 2025. MPAKA WAKATI MWINGINE MIMI NI FRANCO ATILYO**